# KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO

# KONFERENSI YA KASKAZINI MASHARIKI MWA TANZANIA -NETC

## SEMINA ZA KWA VIONGOZI WA KANISA

## MADA: “MALEZI YA WASHIRIKI”


**IMEANDALIWA NA KUSANYWA**

**NA**

**MCHUNGAJI MUSA E. NZUMBI**

**KATIBU MKUU NETC**


**2017**

MALEZI YA WAUMINI - PR MUSA NZUMBI

## MALEZI YA WAUMINI

Semina hii imeandaliwa Kuyasaidia makanisa na viongozi pamoja na Wainjilist Walei Wajue Namna Ya Kulea na kutunza waumini wapya, wa zamani na wanaotarajiwa kuingia kanisani.

**Kauli-Mbiu ya Kanisa la Ulimwengu kwa hii Miaka Mitano ni: "UTUME KWANZA NI -WAKATI WA MAVUNO"**

Kaulimbiu hii inaungana na UTUME WA KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO (Mission Statement) inayosema: "Ni Kuwafanya watu wote kuwa wanafunzi kuwatangazia (communicating) watu wote Injili ya milele katika mukitadha wa ujumbe wa Malaika wa tatu wa Ufunuo 14:6-12, na kuwaongoza wampokee Yesu Kristo kama mwokozi wa maisha yao na kujiunga na kanisa lake, kuwafanya wanafunzi wamtumikiea Yesu kama Bwana na kuwaandaa kwa ajili ya marejeo yake ya haraka"

Tafakari Nukuu hizi za Roho ya unabii zinazoeleza kuhusu Waumini wote kuingizwa kazini kwa ajili ya Utume.

1. "Ni kosa la kutisha kudhania kuwa kazi ya kuongoa roho ni ya wachungaji peke yao" DA 822
2. "Mvua ya masika haitamwagwa sehemu kubwa ya washiriki wasipoingia kazini kuongoa roho" (RH.21/7/1896
3. "Washiriki wetu watakapofanya kazi kwa umoja, chini ya uongozi mmoja kwa kusudi moja la kuongoa roho, wataupindua ulimwengu" 9T.221
4. "Mungu ametuheshimu sana kutufanya watendakazi pamoja naye" 3T.391
5. "Wadhambi wanaoangamia wataendelea kuangamia mpaka watu wawapelekee nuru" 3T 391
6. "Mungu hatatumia malaika toka mbinguni wafanye kazi aliyoiacha kwa wanadamu kuifanya" 3T391
7. "Giza la dunia iliyoharibika linawaita wanaume na wanawake wakristo kuingiza juhudi zao, kila mmoja ili kuirejesha sura ya Mungu iliyopotea kwa wanadamu" 3T391
8. "Kila kanisa ni lazima liwe shule ya kuwafundisha wa washiriki kuwa watendakazi wanaoongoa roho" (C "Kazi ya Mungu hapa duniani haitakamilika hadi pale ambapo wanaume na wanawake wanaounda ushirika kanisani watakimbia kutenda kazi, na kuunganisha juhudi zao pamoja na wachungaji na vioingozi wa kanisa" (Gospel Workers, pp. 351-352). Christian Service, p. 59).
9. "Huduma ambayo ni kubwa zaidi ya zote . . . Ni kuwatoa wanaume na wanawake kutoka katika Mitego ya Shetani na kuwaunganisha na Mungu." 6 T 339
10. "Elimu ya kweli ni mafunzo ya Umishonari. Kila wana na binti za Mungu wameitwa kuwa Wamishonari; tumeitwa kwenye huduma ya Mungu kwa binadamu wenzetu, na ili kufaa kuifanya huduma hii inapaswa kuwa ni lengo la elimu tunayopata. MH 395
11. "Kanisa ni Wakala Mungu aliyewekwa mahususi kwa ajili ya Wokovu wa Watu. Liliwekwa kwa ajili ya Huduma, na kazi yake kubwa ni Kuibeba Injili ya milele kwa Ulimwengu wote" *(The Acts of the Apostles, p. 9)*

MALEZI YA WAUMINI - PR MUSA NZUMBI

**UTUME NA MALEZI**

Kama nukuu hizo hapo juu zinavyojieleza, hakuna shaka kuwa msukumo mkubwa kwa kanisa kwa sasa ni kuwaingiza washiriki wote kazini, hii ni kufuatia msukumo wa kila muumini kuwa mmishonari na kutakiwa anajihusisha kikamilifu katika kazi ya uongoaji roho. Wakati huohuo kasi ya kuongoa roho inapoendelea ndivyo kasi ya kulea inavyopaswa kuwa kubwa, mpango huu umelifikisha kanisa kuwa na mpango mkakati unaoitwa "Total Membership Involvement" TMI (Ushirikishwaji wa Kila Muumini) – Huu ni mpango mahususi wa kila muumini kuingiza juhudi yake, karama na taranta zake katika kazi ya uongoaji wa roho zinazopotea, hii inakwenda zaidi ya mikutano ya hadhara, hii inahusisha Nyanja zote za uinjilisti.

**HALI YA MALEZI YA KANISA LA DUNIANI**

Matokeo ya Utafiti uliofanywa na Idara ya Kumbukumbu na Utafiti wa Kanisa la Wa Adventista wa Sabato Ulimwenguni kupitia kwa Mkurugenzi wa *Archives, Statistics, and Research (ASTR)* wa Kanisa La Waadventista wa Sabato Ulimwenguni, David Trim, mwaka 2015 alitoa taarifa ya utafiti wa malezi ya washiriki iliyoonyesha kuwa katika kipindi cha miaka 50 tangu 1965 hadi 2014 ilionyesha Ubatizo zaidi ya milioni 33.

Ambapo katika jumla hiyo:

I. 57% ni Wanawake
II. 43% ni Wanaume.
III. Huku Milioni 13 wamepotea kwa njia mbalimbali (Trim, 2015).
IV. Zaidi ya 39% ya waliobatizwa waliliacha kanisa.

Takwimu za Walioliacha Kanisa

Mgawanyo wa idadi ya waumini wanavyoliacha kanisa kwa kufuata umri wao ni kama ifuatavyo:

I. Kiasi cha **62.55%** ni vijana (Young Adult),
II. Huku **34.52%** ni umri wa kati (Middle Aged),
III. **1.27%** ni Watoto wasiobatizwa bado (child never baptized) na
IV. **0.13%** ni Wazee (Old Age).

***HITAJI LA MKAKATI WA MALEZI***

*"Kanisa limepewa wajibu mahsusi wa kushughulikia roho zile zilizofuata mionzi ya nuru ya mwanzo iliyopokelewa, na ikiwa washiriki kanisani watazembea wajibu huu, watakuwa wamedhihirisha ukosefu wa uaminifu wao kwa Mungu aliyewapa huo wajibu".—(**Review and Herald, April 28, 1896).***

"Makanisa mengi mahalia yana ukosefu wa utaratibu madhubuti wa kutunza washiriki – hususani kwa wale walio katika hatari ya kuliacha kanisa. Makanisa mahalia yanahitaji

MALEZI YA WAUMINI - PR MUSA NZUMBI

wachungaji wa kuwaandaa wazee wa makanisa na washiriki kwa ujumla kuhudumiana kichungaji kwa kila mmoja” (**GC President’s Report 2015**).

**NJIA MBALIMBALI ZA MALEZI YA WASHIRIKI**

**Zifuataza ni njia mbalimbali zinazoweza kutumika katika malezi ya waumini wapya.**

1 NJIA NO 1: MALEZI KUPITIA BARAZA LA KANISA

Baraza la kanisa linawajibika kikamilifu katika Malezi ya Waumini hii ni kama inavyoelekezwa kwenye Kanuni ya kanisa.

“Kila kanisa halina budi kuwa na baraza linalofanya kazi ambalo wajumbe wake wamechaguliwa katika mkutano mkuu wa kanisa, Shughuli yake kubwa ni malezi ya Kiroho ya Kanisa na Kazi ya Kupanga na Kuendeleza Uinjilisti katika sura zake zote”. Kanuni ya Kanisa Toleo la 18, uk 142.

“Kipengele muhimu kuliko vyote katika ajenda lazima kiwe uenezaji wa injili katika eneo la umisionary la kanisa. Zaidi ya hapo mara moja kila robo mkutano mmoja mzima hauna budi kujielekeza katika mipango ya uinjilisti, baraza litachunguza mapendekezo ya konferensi kuhusu programu na njia za uinjilisti na namna inavyoweza kutekelezwa kikanisa mahalia”. Kanuni ya Kanisa Toteo la 18 Uk 144

Nukuu hizo hapo juu zinaonyesha kuwa kazi kubwa ya baraza la kanisa ni malezi ya Waumini, hivyo ni vyema baraza lijikite katika namna ya kuzuia changamoto hii ya waumini kuliacha kanisa, na inapendekezwa kuwa baraza moja kwa robo mara moja lijikite kwa malezi tu.

2 NJIA NO: 2 KUPITIA KAMATI MALEZI NA UREJESHWAJI (KMU)

Kamati ya Malezi na Urejeshwaji (KMU) Ni kamati maalumu inayopatikana kila ngazi ya Kanisa yaani: General Conference, Divisheni, Union, Konferensi, na Kanisa Mahalia. Kamati hii imeundwa kufuatia kutatua tatizo kubwa la waumini kuliacha kanisa.

**WAHUSIKA WA KAMATI YA MALEZI NA UREJESHWAJI: NGAZI YA UNION**

1. Katibu Mkuu wa Union – Mwenyekiti
2. Mkurugenzi wa Huduma Binafsi – Katibu
3. Mkurugenzi wa Huduma ya Wana wa kike – Mjumbe
4. Katibu wa Huduma za Kichungaji – Mjumbe
5. Mkurugenzi wa Vijana – Mjumbe
6. Mkurugenzi wa Huduma za Watoto – Mjumbe
7. Mwakilishi mmojawa Walei – Mjumbe
8. Mwakilishi mmoja wa Vijana – Mjumbe

MALEZI YA WAUMINI - PR MUSA NZUMBI

## WAHUSIKA WA KAMATI YA MALEZI NA UREJESHWAJI: NGAZI YA KONFERENSI

1. Katibu Mkuu wa Konferensi – Mwenyekiti
2. Mkurugenzi wa Huduma Binafsi – Katibu
3. Mkurugenzi wa Huduma ya Wana wa kike – Mjumbe
4. Katibu wa Huduma za Kichungaji – Mjumbe
5. Mkurugenzi wa Vijana – Mjumbe
6. Mkurugenzi wa Huduma za Watoto – Mjumbe
7. Mwakilishi mmojawa Walei – Mjumbe
8. Mwakilishi mmoja wa Vijana – Mjumbe

## KAMATI YA MALEZI NA UREJESHWAJI: NGAZI YA KANISA MAHALIA

1. **Jina:** Kamati ya Malezi na Urejeshaji (KMU)
2. **Inawajibika Kwa:** Baraza la Kanisa
3. **Wajumbe wake:**
4. Mmojawapo wa wazee wa Kanisa lakini sio mzee kiongozi - **Mwenyekiti**
5. Karani wa kanisa – **Katibu**

## WAJUMBE WA KAMATI YA KMU NGAZI YA KANISA MAHALIA

1. Mzee wa Kanisa – Mwenyekiti
2. Karani wa Kanisa - Katibu
3. Kiongozi Huduma za Wana wa Kike – Mjumbe
4. Kiongozi wa AMO – Mjumbe
5. Kiongozi Huduma za Vijana – Mjumbe
6. Kiongozi wa Huduma za watoto – Mjumbe
7. Wengine wawili au watatu kulingana na pendekezo la kanisa k.m. Mkuu wa Shule ya Sabato, au Shemasi mkuu wa kiume na/au wa kike, n.k.

## MAJUKUMU YA KAMATI HII YA MALEZI NA UREJESHWAJI NGAZI YA KANISA MAHALIA

I. Kutayarisha orodha ya watu wanaohudhuria kanisa mahalia ukiambatanisha maelezo mafupi ya kila mmoja
II. Kuchunguza mwelekeo wa usharika wa kanisa mahalia
III. Kutambua maswala yanayowafanya watu kuacha kanisa kwa kusaidiana na kanisa mahalia
IV. Kupata ufumbuzi wa mambo mbali mbali yanayojitokeza kwa kusaidiana na kanisa mahalia.
V. Kuwasilisha orodha ya changamoto na ufumbuzi wa hizo changamoto katika baraza la kanisa.
VI. Kubuni program, shughuli, maanzisho na dhana zitakazotumika kushughulikia maswala yaliyoletwa na walengwa
VII. Kutekeleza hizo shughuli, program, maanzisho na dhana zilizotayarishwa kupitia katika vyombo vya kanisa viliyoanzishwa sawa sawa na kanuni elekezi
VIII. Kupitia upya maadili na mguso wa program, shughuli, maanzisho na dhana za kiroho kwa kanisa mahalia
IX. Kutathmini program hizo mara kwa mara (kila robo au kila mwaka)
X. Kutayarisha na kutoa taarifa mara kwa mara kwa kanisa kupitia baraza la kanisa
XI. Kuandaa na kupitia orodha ya wote waliobatizwa kwa kuwandika majina, namba za simu, mahali wanapoishi, ili kufatilia kwa karibu mara baada ya ubatizo.

MALEZI YA WAUMINI - PR MUSA NZUMBI

XII. Kuweka mkakati wa timu ya kuwatembelea waumini wote kwa kujua mahali wanapoishi timu hizi zinaweza kuratibiwa na kutoa taarifa ya maendeleo ya kazi hiyo.

3 NJIA NO: 3 KUPITIA IDARA MBALIMBALI ZA KANISA (MF WM, AMO, KAYA NA FAMILIA, WATOTO, VIJANA, CHAPLENSIA NK).

Idara mbalimbali za kanisa zimewekwa ili kuwa vyenzo za kukamilisha utume wa kanisa, hata hivyo moja ya malengo ya kuwa na idara hizi ni kusaidia na kuratibu malezi ya waumini ndani ya idara, hii inafanyika katika muktadha wa kuwasaidia wanaidara kuwa hai katika majukumu ya idara na kuwaunganisha katika kutekeleza utume na kazi ya Mungu katika kanisa mahalia.

Mifano ya Idara zinazoingia mojakwamoja katika malezi ya Wanaidara wake ni pamoja na:

I. Idara Huduma za Kaya na Familia.
II. Idara ya Huduma za Wana wa kike.
III. Idara ya Huduma Binafsi
IV. Chama cha Adventist men organization (AMO)
V. Chama cha Dorkasi.
VI. Idara ya Huduma za Vijana.
VII. Idara ya Chaplensia inayoratibu: Wafungwa, Wanachuo, Wanafunzi, na Wanajeshi
VIII. Chama cha Pathfinders (PFC)
IX. Chama cha Adventurers (AC)
X. Idara ya Huduma za Watoto.

4 NJIA NO: 4 KUPITIA VIKOSI VYA UTENDAJI VYA SHULE YA SABATO.

Vikosi vya utendaji vya shule ya sabato ni moja ya zana muhimu ya malezi ya waumini, hii ni kufuatia ukweli kwamba ni kupitia Shule ya Sabato ndipo waumini wanajengwa katika mahusiano ya muumini na muumini, na pia ni kupitia shule ya sabato ambapo waumini wanauelewa ukweli wa Biblia kwa kujifunza kupitia miongozo ya Biblia.

**Vikosi vya Utendaji vya Shule Ya Sabato (Sabbath School Action Unity) na Malezi ya Waumini.**

i. Idadi ya 6-8 ni namba inayowaweka karibu waumini kwa kufahamiana na kujifunza pamoja, hivyo ni rahisi kufatilia kama kuna mwanakikosi ambaye amepata shida na kutokuhudhuria kanisani kwa ibada.
ii. Vikosi hivi vina Viongozi wake: Mwenyekiti, Katibu, na Mratibu wa Utume. Hawa hushirikiana na kuwasaidia kuongoza wanakikosi hasa kama kuna mwanakikosi amepata shida.
iii. Vikosi hivi huwa na daftari la mahudhurio, daftali hili ni kifaa maalumu sana kwa kuratibu mahudhurio ya kila sabato na kila wanapopanga kukutana.
iv. Mwenyekiti wa Kikosi (kazi yake inaenda zaidi ya kujifunza lesoni), kazi yake ni kuwaunganisha wanakikosi, hapa anapowaunganisha tayari hayo ni malezi.

MALEZI YA WAUMINI - PR MUSA NZUMBI

v. Kikosi hiki cha utendaji kinalenga Kufahamiana na kuweka mikakati peke yao.
vi. Kukidhi malengo 4 ya Shule ya Sabato (Utume, Ushirika, Usomaji, na kuifikia jamii)
vii. Ni rahisi Kufanya ufatiliaji katika kikosi hiki kuliko kanisa zima.

5 NJIA NO: 5 KUPITIA IBADA ZILIZOPANGWA NA ZINAZOVUTIA.

Pale ambapo ibada zimeandaliwa vizuri na kwa ufanisi mkubwa matokeo yake yataonyesha mafanikio ya malezi ya waumini. Ibada hizi ni pamoja na:

i. Ibada ya siku ya sabato
ii. Ibada ya katikati ya juma (Jumatano)
iii. Ibada ya kufungua Sabato (Ijumaa jioni)
iv. Ibada ya kufunga Sabato (Jumamosi jioni)
v. Majuma ya maombi mbalimbali.

6 NJIA NO: 6 KUPITIA VIPINDI VYA SABATO MCHANA VILIVYOANDALIWA NA KUWA NA MADA MBALIMBALI.

7 NJIA NO: 7 KUPITIA HUDUMA YA KUTEMBELEA WAUMINI NYUMBANI NA OFISINI.

8 NJIA NO: 8 KUPITIA WASHIRIKI WAPYA KUINGIZWA KAZINI MARA BAADA YA KUBATIZWA.

9 NJIA NO: 9 KUPITIA MAKUNDI MADOGOMADOGO KANISANI (SMALL GROUPS) 10 KWA 10 KILA KANISA.

10 NJIA NO: 10 KUPITIA KILA MSHIRIKI AINGIZWE KAZINI, (TOTAL MEMBERSHIP INVOLVEMENT TMI)

11 NJIA NO: 11 KUPITIA UINJILISTI KWA KILA MUUMINI.

12 NJIA NO: 12 KUPITIA WABATIZWA WAIVISHWE KIMAFUNDISHO NA KULIELEWA KANISA NA MFUMO WAKE VIZURI.

13 NJIA NO: 13 KUPITIA PROGRAMU YA KUFUASA

**KUFUASA NI NINI? Ni mchakato wa kumfanya mtu kuwa mfuasi wa Kristo kwa kumsaidia akue, atembee, na kutenda kama Kristo.**

*MALENGO YA KUFUASA*

*Kufuasa kama Kristo—kusimika mambo yaliyo na umuhimu wa kuendelea kukua kiroho na maendeleo miongoni mwa wale waliompokea Kristo kama Bwana na Mwokozi, kulea na kufundishana kila mmoja katka maisha ya haki, kutoa mafunzo kwa ajili ya ushuhudiaji wenye ufanisi, na kutia moyo kuwajibika kutii mapenzi ya Mungu ((ECDWP, A(3) 2015).*

**TAFASIRI YA WANAFUNZI NA KUFUASA**

MALEZI YA WAUMINI - PR MUSA NZUMBI

**Mwanafunzi-** mmoja aliyeweka imani yake ndani ya Kristo kwa ubatizo, amejitambulisha mwenyewe kama mwanafunzi wa Kristo na mjumbe wa kanisa la Kristo.

**Kufuasa-** utaratibu wa kanisa, kwa mamlaka na uwepo wa Kristo, linakuwa chanzo cha: kuwaongoza watu kwenye imani na kujitoa kwa Kristo, kuwashirikisha kwa Kristo na jumuiya yake ya agano, kupitia ubatizo, kuwaongoza kwenye maisha ya utii wa mapenzi yote ya Kristo, na Kuwarejesha zizini kondoo wote waliotanga mbali na kuliacha kundi kwa sababu mbalimbali.

MISINGI YA KUFUASA

- Kufuasa ni moyo wa utume wa Kristo na kanisa
- Kufuasa ni tamko lake la utume
- Tamko lake la utume lina ahadi ya uwepo wake

SABABU ZA KUFUASA

- Kuliandaa kanisa la Kristo
- Kumfanya Bibi Arusi kustahili kwa Bwana Arusi

WAJIBU WA KANISA KATIKA KULEA NA KUTUNZA WAUMINI WAPYA

- Kuweka Mipango
- Njia Za Kufuasa

I. Kufuasa kwa njia ya ukuaji binafsi wa kiroho
II. Kufuasa kwa njia ya kuwa kielelezo katika upendo
III. Kuwashirikisha katika huduma za kanisa

**Kurejesha Waumini Waliopoa na Waliorudi Nyuma**

1. Kuwatafuta
2. Kuwaleta
3. kuwatunza

KUFUASA KWA MPANGO WA MAKANISA MADOGO

**Maana ya Makanisa Madogo na Makubwa**

- ✓ Kuna makanisa makubwa na kuna makanisa madogo.
- ✓ Kanisa lenye washiriki 25-**35**-50— Ni kanisa la kifamilia. Mahudhurio 35.
- ✓ Kanisa lenye washiriki 51-**110**-150—Ni kanisa lenye timu moja. Mahudhurio 110.
- ✓ Kanisa lenye washiriki 151-**250**-350—Ni kanisa lenye vikundi au tabaka nyingi ndani yake. mahudhurio ni washiriki 250.
- ✓ Kanisa lenye washiriki 351-**600**-900—Hili ni kanisa kubwa, mahudhurio ni watu 600 kwa kila sabato.
- ✓ Kanisa lenye washiriki 901-**2000**- au zaidi—Ni kanisa kubwa kupindukia(A mega-church). Ni kanisa gumu kuongozwa na mchungaji mmoja.

MAKANISA NA IDADI YA WAUMINI

MALEZI YA WAUMINI - PR MUSA NZUMBI

Makanisa yenye wastani wa mahudhurio ya waumini 35 hadi 110 yana sifa ya kuwa **madogo.** Yale yenye mahudhurio kuanzia 250 hadi 2000 yana sifa ya kuitwa **makanisa makubwa.** Kulea waumini wapya katika makanisa haya kila moja lina changamoto zake

KUFUASA KWA NJIA YA KUPANDA MAKANISA MADOGO

**Vikwazo vya makanisa makubwa katika kufuasa**

- Makanisa makubwa yana mashindano mengi ya madaraka, kugombea nafasi za kudhihirisha karama zao na mengineyo.

- Makanisa makubwa hayana viti vya kutosha, jengo la kutosha la ibada wala waalimu wa kuwasaidia waumini wengi wapya.

FAIDA ZA MAKANISA MADOGO

1. Ibada zinazoendeshwa na makanisa madogo zina usikivu na urafiki
2. Washiriki wanaweza kusemezana, kukaribishana kila mmoja na kuonyeshana wema.
3. Viongozi ni marafiki tofauti na wa makanisa makubwa ambao hutumia nguvu na muda mwingi kuonyeshana ubabe na kugawa washiriki.
4. Viongozi huweza kusemezana wazi kwa jambo lolote walipatalo kuwa lina msaada.
5. Swala la utambuzi wa wageni wapya wanaowafikia kanisani ni rahisi kwao kuliko makanisa makubwa.
6. Ujenzi na utunzaji wa majengo ya makanisa madogo na vifaa pia una gharama ya chini.
7. Ugomvi wa elimu ya kitheolojia haupo katika makanisa madogo.

**MWISHO**

MALEZI YA WAUMINI - PR MUSA NZUMBI